# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU
## KAZI, VIJANA, AJIRA NA MAHUSIANO

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA KINGA YA JAMII

**06 Februari 2026, Dodoma**

Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano inaujulisha Umma wa Watanzania kuwa Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya mwaka 2023 na Skimu ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii kwa Wananchi Wanaojiajili katika Sekta Isiyo Rasmi (NISS) zitazinduliwa rasmi tarehe 09 Februari, 2026 wakati wa Mkutano wa Wadau Sekta ya Kinga ya Jamii unaotarajiwa kufanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) jijini Arusha tarehe 09 hadi 10 Februari, 2026.

Pamoja na uzinduzi wa Sera na Hifadhi Skimu, wadau wa Sekta ya Kinga ya Jamii, watajadili maendeleo na fursa zinazopatikana katika sekta hiyo. Mkutano huu utakutanisha Wadau wa Kinga ya Jamii wapatao 1,200 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kauli Mbiu ya Mkutano huu ni "**Kinga ya Jamii kwa Wote, Msingi wa Maendeleo".**

Imetolewa na;

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**